

## Kanisa La Kristo Sio Dhehebu - 1

Fedha tunazotumia zimegawanyika katika aina tofauti, 10,000/-, 5,000/-. Na taratibu za siasa zimegawanyika, CCM, TLP. Kwa hiyo tunaona kuititia mifano kwamba neno “dhehebu” ni magawanyiko au kundi fulani. Katika ulimwengu wa dini, “Dhehebu” ni jamii ya watu waliotengana na Kanisa lilianzishwa na Kristo. Ndiyo katika Agano Jipy Biblia inazugumza kuhusu makusanyiko (1 Kor. 1:2) au Kanisa zima (Efe. 1:22-23). Lakini wale watu kwenye makusanyiko walikuwa Wakristo katika Kanisa la Kristo. Hawakuwa Walutheri katika Kanisa la Moravian.

### I. Kanisa La Kristo Ndilo Kanisa la Karne ya Kwanza.

- A. Tuangalie yaliyo kweli.
  1. Kanisa la Kristo siyo Kanisa la Wayahudi.
    - a. Agano la Kale, msingi wa Wayahudi ultolewa, Rum. 7:1-4; Kol. 2:14-17; Ebr. 8:8-13.
  2. Kanisa la Kristo siyo “Protestant” kundi la watu waliochukia na mafundisho ya Katoliki kwa hiyo wakaacha kusali na wakaanzishwa makanisa yao.
    - a. Madhehebu yote yalianzishwa baada ya karne ya kwanza na kama kuna kundi la watu walianzisha bada ya karne la kwanza na wanadamu, basi hawa watu hawawezi kuwa Kanisa lilojengwa na Kristo.
    - b. Kanisa la Bwana wetu alilianzishwa katika karne ya kwanza mwaka wa 33, Marko. 9:1; Mdo. 1:8; Mdo. 2:1-4, 47.
  3. Vitendo vya madhehebu havimo katika Kanisa.
    - a. Madhabahu ya maombi.
    - b. Kupiga kura kwa watu wanaotaka kuijunga.
    - c. Vyombo vya muziki.
  4. Kanisa la Kristo sio Kanisa la Katoliki.
    - a. Kanisa la Katoliki lilianzishwa katika mwaka wa 606 Bk, karibu na miaka 600 baada ya maisha ya Yesu.
    - b. Na tukiangalia mafundisho ya Wakatoliki tutaona kwa ufupi hawapati mamlaka yao kutoka kwa Mungu.

### II. Fafanuzi ya Kanisa.

- A. Neno “Kanisa” limetoka kwenye neno ya Kiyunani “Ecclesia,” na maana yake ni “Walioitwa”.
  1. Kwa hiyo Kanisa ni mwili wa watu walioitwa kutoka ulimwenguni, 2 Thes. 2:14.
    - a. Kwa kutii injili, 2 Thes. 1:7-9.
  2. Kanisa linaongozwa na Kristo, kichwa cha Kanisa lake, Kol. 1:18.
  3. Na Roho anakaa ndani ya Kanisa, Efe. 2:22-23.
- B. Kanisa ni moja katika hesabu.
  1. Yn. 10:16, Kuna kundi ngapi? \_\_\_\_\_
  2. Na Kanisa ndiyo kundi lile, Mdo. 20:28.
  3. Tena kuna mwili moja, Efe. 4:4.
  4. Na mwili ni Kanisa, Efe. 1:22-23.
  5. Tunajua Yesu alifundisha kuhusu ndoa tunaweza kuwa na mke moja tu, Mat. 19:1-9; Rum. 7:1-4.
  6. Na Kanisa ni mke wa Yesu, Efe. 5:22-23.

### Hitimisho:

Tutaendela kujifunza kuna Kanisa moja tu. Wazo la Kanisa moja naona tumeelewa. Lakini labda tumeelewa kwa maneno na siyo kwa matendo kwa sababu mara nyingi watu wanaanguka na wanajiunga na

madhebu. Kwa maana hawakuelewa vizuri mafundisho ya Kristo ndiyo maana wanapotea.